Journal Homepage: -www.journalijar.com

INTERNATIONAL JOURNAL OF ADVANCED RESEARCH (IJAR)

ISSN NO. 2320-5407

**Article DOI:**10.21474/IJAR01/5735
**DOI URL:** http://dx.doi.org/10.21474/IJAR01/5735

***RESEARCH ARTICLE***

# UHUSIANO WA MBINU ZA KUFUNDISHA SARUFI NA UMILISI WA MAZUNGUMZO YA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI ZA UMMA, KAUNTI NDOGO YA KISUMU MASHARIKI.

**Mrs Hellen Wambui.**
Department of Educational Communication & Technology University of Nairobi.

## Manuscript Info

***Manuscript History***

Received: 01 September 2017
Final Accepted: 03 October 2017
Published: November 2017

***Key words:-***
Pragmatiki, sarufi, sintaksi, semantiki, ufundishaji.

## Abstract

Lugha ya Kiswahili kina dhima kubwa ulimwenguni katika kukidhi mahitaji ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kielimu. Nchini Kenya, Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi. Isitoshe, Kiswahili ni somo la lazima linalofundishwa na kutahiniwa katika viwango vya shule za msingi na sekondari. Msingi wa lugha hii ni sarufi ambayo hutawala stadi zote za lugha. Licha ya dhima ya sarufi katika kufanikisha mawasiliano tafiti nyingi zinaonyesha kuwa wanafunzi wengi hawawezi kujieleza kwa usahihi na kwa ufasaha hata baada ya kuhitimu masomo ya msingi. Hali hii ilimchochea mtafiti wa kazi hii kuchunguza uhusiano uliopo kati ya mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi.Utafiti huu ulidhamiria kutimiza lengo lifuatayo: Kuchunguza mbinu zinazotumiwa na walimu kufunza sarufi ya Kiswahili. Utafiti huu ulifanyika katika Kaunti ndogo ya Kisumu Mashariki. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mfumo katika utaratibu wa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili.Muundo wa kimaelezo ulitumika. Mtafiti alitumia uteuzi sampuli kinasibu kuteua shule katika viwango vya kitaifa, kaunti na kaunti ndogo.Uteuzi makusudi ulitumika kuteua darasa la saba na walimu wao. Sampuli lengwa ya wanafunzi iliteuliwa kinasibu.Data ilikusanywa kutumia hojaji, mahojiano na utaratibu wa utazamaji darasani ili kuimarisha uaminifu na uthabiti wa data.Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa muundo wa kimaelezo,kithamani na kiidadi.Data hii iliwasilishwa kwa kutumia majedwali na grafu.Matokeo yalionyesha kuwa walimu wengi walitumia mbinu ya mhadhara katika kufundisha sarufi huku mbinu za kisasa zinazowashirikisha wanafunzi zaidi zikipuuzwa.Utafiti pia ulidhihirisha kuwa wanafunzi hawashirikishwi ipasavyo katika mazoezi yanayoweza kuimarisha umilisi wa sarufi na mazungumzo.Isitoshe,matumizi ya chaki na ubao ulitawala utaratibu wa kufundisha sarufi huku vifaa vingi vikikosa kutumika.Hatimaye utafiti huu ulibainisha kuwa kuna uhusiano kati ya mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi.Utafiti huu ulipendekeza kuwa kuwepo na mafunzo kwa walimu kuhusu mbinu,mazoezi na vifaa mwafaka katika ufundishaji wa sarufi ili kuimarisha umilisi wa lugha ya Kiswahili.

*Copy Right, IJAR, 2017,. All rights reserved.*

**Corresponding Author:-Hellen Wambui.**
Address:-Department of Educational Communication & Technology University of Nairobi.

# Introduction:-

## UTANGULIZI

Ulimwenguni kote, lugha huchukuliwa kuwa sehemu muhimu katika maisha ya mwanadamu kwani huwa ndiyo chombo cha mawasiliano. Lugha huwawezesha watu kuwasilisha hisi zao, mambo wanayoyapenda na wasiyoyapenda (Crystal, 1997). Lugha huwa chombo chakubadilisha maadili, mielekeo na matarajio ya watu walio na utamaduni unaowatambulisha (Trudgil, 1983).

Dhima ya lugha ulimwenguni imeibua haja ya kuimarisha mbinu za ufundishaji wa lugha na nyenzo za kufundishia lugha (Richards na Rodgers, 2001). Mfano mzuri ni lugha ya Kiswahili ambayo imepanuka katika matumizi yake kutoka karne ya 19 hadi sasa katika Afrika mashariki na ya kati na hata ng'ambo na kuwavutia wasomi, watafiti, wanaisimu, wanajeografia na wanahistoria (Chimera, 2000).

Kwa muda mrefu Lugha ya Kiswahili imechangia katika kukidhi malengo ya kisiasa, kiuchumi, kitamaduni, kijamii na elimu. Jambo hili limeipa hadhi lugha ya Kiswahili kiasi cha kutambulika miongoni mwa lugha saba za kimataifa katika karne ya 21 (Chiragdin na Mnyampala, 1977). Nchini Kenya, umaarufu wa lugha hii umepiga hatua kubwa katika viwango vya kitaifa na elimu. Jambo hili limesababisha wakuza mtaala na waundaji sera kufanya mabadiliko ili kuinua hadhi ya lugha hii ili kukidhi mahitaji yanayozidi kuongezeka.

Mifano ya hatua hizo za kukikuza na kukiendeleza Kiswahili ni Ripoti ya Ominde (1964) iliyotambua majukumu mawili ya lugha ya Kiswahili. Kwanza kama chombo cha kuwaunganisha wananchi na pili kama Lingua Franka katika mawasiliano barani Afrika.

Kamati ya kitaifa kuhusu malengo na sera za elimu (Gachathi Report 1976) ilitoa mapendekezo kuwa Kiswahili kiwe somo la lazima katika shule za msingi na za upili.

Kufuatia mapendekezo ya Ripoti ya MacKay (1981), mfumo mpya wa Elimu (8-4-4) ulianzishwa na mtaala wa lugha ya Kiswahili kwa shule za upili ukabadilika kwa kiwangokikubwa. Jambo hili lilinuia kuwapa wanafunzi uwezo na maarifa yatakayo wafaa shuleni na katika maisha ya baadaye. Kwa mara ya kwanza, ripoti hii ikapendekeza kuwa Kiswahili kiwe somo la lazima na la kutahiniwa.

Silabasi ya Kiswahili (1985) ilitilia mkazo ufundishaji wa stadi za kuzungumza na kusikiliza ambazo hazikushughulikiwa hapo awali. Hatua hii ilishinikiza kushirikisha kwa sauti au foni zilizozua utata katika matamshi ya wazungumzaji wa jamii mbalimbali kwa kusudi la kuboresha mazungumzo.

Mapitio ya mtaala wa Kiswahili ya 2002 yalikuwa muhimu zaidi kwani yalilenga kuinua hadhi ya Kiswahili na matokeo yake katika mitihani. Kufuatia mapitio haya, kulikuweko na ongezeko la vipindi vya Kiswahili kutoka vitano hadi sita katika shule za msingi. Uhakiki huo pia ulisababisha ufasili na utekelezaji wa masuala yaliyokuwa na utata katika sarufi. Kwa mfano, uanishaji wa ngeli za Kiswahili ambazo ndio uti wa mgongo wa sarufi ya Kiswahili (Mbaabu, 1995).

Aidha, mapitio haya ya usawazishaji wa silabasi yalipendekeza mbinu za ufundishaji wa Kiswahili ambazo zingeboresha ufundishaji na kutimiza malengo ya elimu nchini katika kufaulisha mawasiliano na ufasaha wa lugha. Ili kutimiza azma hii, mapitio haya yalipendekeza mbinu ya mwingiliano inayomtazama mwanafunzi kama kiini cha ufundishaji.

Katiba ya Kenya (2010:20) ilikipa Kiswahili hadhi zaidi kwa kukitambua kama lugha ya taifa na rasmi. Kwa sasa, Kiswahili kinatarajiwa kutumika kama chombo cha mawasiliano katika taaluma mbalimbali kama vile utawala, na taasisi mbalimbali kama vile bunge na mahakama. Kutokana na mchakato huu, ni wazi kwamba maarifa mema ya lugha ya Kiswahili hayawezi kuepukika.

Jinsi ya kukikuza na kukiendeleza Kiswahili limekuwa suala la kuwahusu wanaelimu na pia watafiti. Kwa mfano, kwa mujibu wa Babusa (2010), Abigael (2000), Mbaabu (2003) na Mwihaki (2006), umilisi wa Kiswahili hutegemea aina za shule, mbinu za ufundishaji na mielekeo ya wanafunzi kwa lugha ya Kiswahili.

Huwenda kukawa na vigezo vingi vinavyochangia kudidimia kwa hadhi ya Kiswahili sanifu nchini kama inavyodhihirika. Licha ya ukweli huu, uchunguzi huu ulizingatia mbinu zinazotumika katika kufundisha sarufi ya

Kiswahili kama mojawapo wa kisababishi cha kuzorota kwa lugha sanifu. Hili ni muhimu kutokana na ukweli kuwa sarufi huchukuwa nafasi muhimu katika lugha.

Kwa mujibu wa Lilian na Bwire (2008), sarufi ni kiambajengo muhimu cha lugha. Mwanafunzi anahitaji muundo (maneno, virai, na sentensi) na sheria zinazotawala habari na matumizi yazo katika utekelezaji wa stadi nne za msingi za lugha. Wataalamu Williams (2005), Larnisen (2003) na Gathumbi na Masembe (2005) wanaunga mkono hoja hii wanaposema kuwa kusanifisha sarufi kunaimarisha stadi za kusikiliza, kuzungumza na kuandika na hivyo kumpa mwanafunzi umilisi wa lugha kwa jumla.

Ili lugha sanifu na sahihi kutumika, lazima sarufi ya lugha hiyo izingatiwe. Sarufi inahifadhi lugha safi kama inavyozungumzwa na wazawa wa lugha walio na umahiri wa lugha hiyo (Mbaabu, 1985). Kutokana na dhima kuu ya sarufi kwa lugha, umilisi wa kisarufi ndio kiini cha vitabu vingi vya lugha vya kisasa (Richards, 2001). Katika vitabu hivi vya mazoezi ya Kiswahili, sheria za kisarufi huwakilishwa kwa upande mmoja na mazoezi yanayotumia sheria hizi kwa upande mwingine.

Kutokana na dhima kubwa ya mbinu za kufundisha lugha katika kufanikisha umilisi wa lugha na mawasiliano kwa muda mrefu wasomi na watafiti wamekuwa wakijishughulisha na tatizo la kuboresha mbinu hizi. Swala hili ndilo msingi wa utafiti huu.

**Lengo la utafiti:-**

Mojawapo ya madhumuni ya kufundisha Kiswahili katika kiwango cha shule za msingi ni kumpa mwanafunzi umilisi wa kudumu wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika (Silibasi ya Kiswahili, 2002). Hata hivyo, wanafunzi wengi hawawezi kujieleza kwa usahihi na ufasaha hata baada ya kuhitimu masomo ya msingi. Wengi wao hufanya makosa ya kisarufi yanayodhihirika katika mazungumzo na maandishi. Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa hali hii huweza kuwa imechangia katika kuzorota kwa hadhi ya Kiswahili sanifu pamoja na matokeo mabaya katika mitihani ya Kiswahili ya kitaifa nchini Kenya (Mwihaki, 2006; Mbaabu na Nzunga, 2008; Fink, 2005; Wairimu, 2000; Daily Nation December 29, 2012; Daily Nation February 29, 2012).Kufuatia hali hii ya kusikitisha, utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo kuna uhusiano wowote kati ya mbinu za ufundishaji wa sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi.

**Kusudi la utafiti:-**

Kusudi la utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza uhusiano uliopo kati ya mbinu zinazotumika kufunza sarufi ya Kiswahili na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulichunguza mbinu za ufundishaji sarufi.

**Umuhimu wa uchunguzi:-**

Matokeo ya utafiti huu na mapendekezo yake yataongeza maarifa katika mbinu za ufundishaji wa sarufi zinazotumiwa na walimu wa lugha ya Kiswahili kwa matumaini ya kuimarisha umilisi wa mazungumzo ya Kiswahili sanifu na matokeo ya mitihani ya kitaifa.

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya msaada kwa wakuza mtaala ambao watayatumia katika kuunda mtaala utakaoafikiana na yaliyomo katika silabasi, mbinu za ufundishaji na vyombo vya kufundishia sarufi. Waandishi wa vitabu vya kiada watapewa mwelekeo ufaao katika uteuzi wa yale yatakayosawiriwa katika vitabu hivi ili kufanikisha uzungumzaji katika Kiswahili.

Matokeo haya pia yatahimiza Wizara ya Elimu kuandaa mafunzo kwa walimu ili kuwapa mafunzo kuhusu mbinu mwafaka za kufundisha sarufi ili kuimarisha umilisi katika mazungumzo ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu pia yataweza kutumika kuondoa mielekeo hasi miongoni mwa wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili na kuzungumza Kiswahili sanifu.

**Upeo na upungufu wa utafiti:-**

Sampuli ya utafiti huu ni ndogo kwani ilihusisha walimu na wanafunzi wa darasa la saba wa shule zilizoteuliwa katika kaunti ndogo ya Kisumu Mashariki. Sampuli hii yaweza kuwa na upungufu kwani mbinu zinazotumika kufunza Kiswahili huenda zikawa tofauti katika darasa mbalimbali na sampuli kubwa. Kwa hivyo, sampuli hii huenda isiafiki shule zote za msingi nchini.

**Muundo Na Njia Za Ukusanyaji Data:-**

**Muundo wa utafiti:-**

Uchanganuzi wa data ya utafiti huu uliongozwa na muundo wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), utafiti wa kimaelezo unaweza kutumika kufafanua mielekeo ya watu, maoni na tabia zao au kuelezea maswala ya kielimu na kijamii. Muundo huu ni mwafaka kwa utafiti huu kwa sababu utamsaidia kuchunguza mbinu zitumikazo kufundisha sarufi na athari zake katika mazungumzo ya wanafunzi. Utafiti huu kwa kiasi kikubwa ulitumia uchanganuzi wa kithamani kuchambua vigezo muhimu vya utafiti na kuimarisha matokeo ya data kwa kutumia uchanganuzi wa kiidadi.


**Eneo la utafiti:-**

Utafiti ulifanywa katika Kaunti ndogo ya Kisumu Mashariki, katika Kaunti ya Kisumu, Nchini Kenya. Sababu ya kuchagua eneo hili ni kuwa hakuna utafiti ujulikanao kuhusu uhusiano wa mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo miongoni mwa wananafunzi uliofanywa hapa. Mbali na hayo, kaunti ya Kisumu ina mchanganyiko wa aina mbalimbali za shule. Hili lilimwezesha mtafiti kutambua mambo yanayoathiri mbinu za ufundishaji katika shule hizi tofauti ili kuibuka na matokeo yanayoweza kutegemewa kuhusu swala la utafiti.

**Matokeo Ya Utafiti:-**

**Majibu ya hojaji:-**

Walengwa katika utafiti huu walikuwa ni watu 296 ambapo tulilenga sampuli ya watu 42 katika shule za mshingi kama ilivyo kwenye Grafu 1.1 ufuatao




1.1: Kima cha majibu ya wanafunzi

Kulingana na matokeo katika Grafu 1.1, kulikuwa na majibu 35 kutoka kwa wanafunzi kudhihirisha asilimia 83 ya kujibu maswali. Walimu 10 waliohojiwa walijibu kuonyesha asilimia 100.Kiwango cha kujibu maswali ya utafiti huo yalikidhi mapendekezo ya wataalamu kama vile Mugenda na Mugenda (2003) na Orodho (2003) waliothibitisha kwamba majibu ya utafiti yanayozidi asilimia 50 yanatosheleza uchanganuzi wa takwimu yoyote ile.

**Demografia na wahojiwa:-**

Kama jambo muhimu katika somo lolote lile, ilikuwa muhimu kutambua sifa za demografia ya wahojiwa. Kulingana na wataalamu kadhaa kama Mugenda na Mugenda (2003), Kothari (2004) na Orodho (2003).Demografia ya wahojiwa hutoa matokeo yanayoweza kutegemewa kwa kukipa kila kipengele uhalisia unaofaa. Matokeo haya yanaweza kulinganishwa na idadi nzima ya watu kwa sababu sifa za sampuli iliyotumika ni kielelezo mwafaka cha idadi hiyo.

Matokeo yalionyesha kuwa kulikuwa na asilimia 62.9 ya wanaume na asilimia 33.1 ya wanawake katika watu waliohojiwa. Matokeo ya Grafu 1.1 yanadhihirisha kuwa kulikuwa na sehemu mbili za kukadiria wastani kwenye matokeo hayo.Sehemu ya kwanza ilikuwa kati ya alama 51-60 na n yingine ikawa kati ya 71-80. Hii iliweza kukadiriwa kuwa alama asilimia 55 kwa kila mwanafunzi katika darasa husika.

Miongoni mwa walimu waliohojiwa, asilimia 80 walikuwa wa kike na asilimia 20 wa kiume. Hii ilikuwa kinyume na idadi ya wanafunzi ambao awali wa kike walikuwa asilimia 33.1 na wa kiume asilimia 62.9. Ingawa matokeo

haya hayatusaidii sana kutoa maamuzi ya utafiti huu, yanaweza kuchangia kuelewa demografia ya idadi ya walimu kwa wanafunzi kwa tafiti zinginezo.

Utafiti huu pia ulizingatia kubaini mielekeo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Matokeo yalikuwa kama inavyoonyeshwa katika jedwali 1.2;

**Jedwali 1.2:-** Mielekeo ya wanafunzi kuhusu ujifunzaji wa somo la Kiswahili

| **Mwelekeo** | **Marudio** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Rahisi | 13 | 37.1 |
| Wastani | 18 | 51.4 |
| Ugumu | 4 | 11.4 |
| **Jumla** | **35** | **100.0** |


Matokeo haya yalionyesha kuwa asilimia 37.1 walipata Kiswahili kuwa rahisi kuelewa huku asilimia 51.4 wakasema ilikuwa wastani nayo asilimia 11.4 wakasema Kiswahili kilikuwa kigumu. Matokeo haya yanawiana na maoni ya watalamu kama vile, Mgullu (1999), Larsen-freeman (2003) na Momanyi (2007) waliodai kuwa ingawa Kiswahili kinazungumzwa na zaidi ya asilimia 80 ya watu wa Afrika Mashariki, wengi wao walishindwa kuzungumza Kiswahili sanifu.

**Mbinu za kufundisha sarufi ya Kiswahili :-**

Data kuhusu mbinu za kufundisha sarufi ilikusanywa kutoka kwa hojaji za walimu na utaratibu wa utazamaji darasani.Kipimo cha linkert kilitumika, ambapo 1 kwenye kipimo hicho ilionyesha mbinu iliyotumika zaidi na 3 ilionyesha mbinu ambayo haikutumika sana.

**Jedwali 1.3:-**Mbinu za kufundisha sarufi ya Kiswahili

| **Mbinu** | **Kiwango** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Chini** | **Juu** | **Wastani** | **Mchepuko** | **Asilimia** |
| Majadiliano | 1 | 3 | 1.51 | .658 | 23.7 |
| Mjadala | 1 | 3 | 1.54 | .701 | 25.2 |
| Maigizo | 1 | 3 | 1.60 | .695 | 24.9 |
| Maswali/majibu | 1 | 3 | 2.00 | .728 | 26.2 |




Matokeo katika grafu hii yanaonyesha kuwa majadiliano ya makundi ndiyo mbinu iliyopendelewa zaidi katika kufundisha sarufi ya Kiswahili ikiwa na kiwango cha asilimia 23.7 ikifuatiwa na maigizo iliyokuwa na kiwango cha chini asilimia 24.9 na kisha mjadala I kiwa na asilimia 25.2. Mbinu ambayo haikutumika sana kulingana hojaji za walimu ni maswali na majibu ikiwana asilimia na 26.2. Mbinu hizi ziliibuka kuwa ndizo hupendwa sana na wanafunzi katika mazoezi yao kama ilivyokuwa imebainishwa na wataalam Bwire na Vikiru (2008) na Brown (2007) ambao walisema kuwa mbinu hizi huwawezesha wanafunzi kuingiliana na kutagusana kuelezea hisia,maoni matamanio na tajiriba zao.Ingawa mbinu hizi zilifurahiwa na wanafunzi utazamaji darasani ulionyesha kuwa walimu

wengi hawakuzitumia bali wengi walitumia mbinu ya mhadhara ambapo mwalimu hutawala mazungumzo. Hali hii inaathiri umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi.

**Muhtasari na hitimisho la matokeo:-**

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza iwapo kuna uhusiano kati ya mbinu za kufundishia sarufi ya Kiswahili na umilisi wa mazungumzo miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Sampuli ilichukuliwa kutoka kwa shule zote, kaunti ndogo ya Kisumu Mashariki, katika. Lengo kuu lilikuwa ni kubaini mbinu vilivyotumika kufundishia sarufi kwa nia ya kuimarisha umilisi wa uzungumzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na hatimaye kuboresha matokeo ya mitihani ya kitaifa ya Kiswahili nchini. Hili lilifanywa kwa kushughulikia vigezo muhimu vya utafiti kama inavyodhihirika hapa.

**Mbinu za kufundisha sarufi ya Kiswahili:-**

Katika hojaji za walimu, wengi wao walidai kuwa walitumia mbinu mbalimbali katika ufundishaji wa sarufi. Miongoni mwa mbinu walizotaja zilikuwa mbinu ya makundi, maswali na majibu, majadiliano na uigizaji.Hata hivyo katika utazamaji wa utaratibu wa kufundisha darasani ilidhihirika kuwa walimu wachache mno ndio waliotumia mbinu zilizotajwa hapo juu. Wengi wao walitumia mbinu ya mhadhara katika ufundishaji. Katika mbinu hii hakukuwa na mtagusano wa kutosha kati ya walimu na wanafunzi hivyo kuwanyima wanafunzi nafasi ya kufanyia mazoezi sheria za sarufi walizofundishwa katika miktadha ya mazungumzo halisi. Hili lilidhihirika kuathiri umilisi wa mazungumzo halisi.

Kama wanavyoshadidia Allwright na Barley (1991) mtagusano kati ya msikilizaji na mzungumzaji huimarisha ujifunzaji lugha. Ellis (1994) pia anasema kuwa mtagusano wa mwalimu na mwanafunzi huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili na huwapa msamiati wa kutumia wakati wa mazungumzo.

Baadhi ya walimu walidai kuwa hawakuweza kushirikisha mbinu tofauti kwa sababu walikumbwa na changamoto kama vile vipindi vichache vilivyotengewa somo la Kiswahili, silibasi pana, na wanafunzi wengi madarasani mwao. Miongoni mwa walimu walioshirikisha mbinu tofauti katika ufundishaji walidai kukumbwa na matatizo yafuatayo; ukosefu wa motisha na ukosefu wa umilisi wa lugha miongoni mwa wanafunzi.

Licha ya changamoto hizi ilibainika wazi ni muhimu kushirikisha mbinu tofauti zitakazowapa wanafunzi nafasi ya kufanyia mazoezi sheria za sarufi walizojifunza ili kuimarisha umilisi wa mazungumzo.

**Mapendekezo :-**

Ilipendekezwa kuwa walimu waimarishe mbinu wanazotumia. Mbinu hizi ziwe ni zile zinawashirikisha wanafunzi zaidi. Miongoni mwa mbinu hizi ni;mbinu ya makundi, mijadala, uigizaji na majadiliano ambazo kulingana na Littlewood(1981) zinaimarisha umilisi wa mazungumzo. Katika mbinu zote mwalimu awe mwelekezi huku wanafunzi wakiwa ndio kiini cha mazungumzo. Ilipendekezwa pia kuwa muda wa kufundisha Kiswahili uongezwe ili kuwezesha mbinu tofauti kutumika.

**Marejeleo:-**


1. Abigael W. M. (2000). *Factors influencing the performance of Kiswahiliin KCPE in Dagoreti Division*, NairobiProvince. Unpublished MED Thesis; KenyattaUniversity.
2. Babusa H. (2010). *Uchanganuzi linganuzi wa mielekeo na umilisi wa lugha ya Kiswahili wa wanafunzi katika mikoa ya Pwani na Nairobi nchini Kenya*. Unpublished PHD. Thesis. KenyattaUniversity.
3. Bwire A.M. na Vikiru L.I. (2008). *Approaches to the Teaching of Grammar and Vocabulary in Groenewegen Bencharks for English language Education*, Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.
4. Crystal D. (1997). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: CambridgeUniversity Press.
5. Chimerah R. (1995). *Kiswahili past present and Future Horizons.*NairobiUniversity Press.
6. Chiragdin, S. na Mnyampala (1977). *Historia ya Kiswahili*: Oxford University Press.
7. Ellis, R. (1994). *The study of second language Acquisition*. London: OxfordUniversity Press.
8. Gathumbi A. na Masembe, S. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
9. Larnisen, F. D. (2003). *Teaching language: From grammar to grammaring*. Boston: Heinle and Heinle.
10. Littlewood, W. (1981). *Communicative Language Teaching – An introduction*. Cambridge: CambridgeUniversity Press.

11. Mbaabu, I. na Nzunga M. (2008). *Sheng' its major characteristics and impact in standard Kiswahili and English*. Dar es salaam. TUKI.
12. Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya publishing and Book Marketing Company Ltd.
13. Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa makosa katika Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.
14. Mckay S. (1985). *Teaching Grammar:* Form 1 Function and Techniques. New York: Pergamon Press
15. Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers, Nairobi.
16. Momanyi, C. (2007). *"Nafasi ya Kiswahili katika Elimu ya vyuo vikuu nchini Kenya" katika Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Kolbe Press.
17. Mugenda, O.M. na Mugenda A.G. (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
18. Mwihaki, A.N. (2006). *"Sheng" na usomi wa Kiswahili, mtazamo wa kiisimu na Jamii*. Makala ya semina ya Isimu jamii ambayo ilitolewa mjini Nakuru. Haijachapishwa.
19. Orodho, J.A. (2003). *Teachniques of Writing Research Proposal and Reports in Education and Social Sciences.* (2nd Ed.) Kanezja HP. Enterprises, Nairobi.
20. Republic of Kenya (1964). *Kenya Education Commisssion Report* (The Ominde Report). Nairobi: Government Printer.
21. Republic of Kenya (1976). *Report of the National committee of Educational policies and objectives* (Gachathi Report), Nairobi: Government Printer.
22. Kombo, D.K. na Tromp, D.L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing:* Nairobi: Paulines Publications Africa.
23. Williams J. (2005). *Form-focused instruction. In E. Hinkel (Ed). Handbook of research in second language teaching and learning*. Mahwah. NJ: Lawrence Erlbaum Associates.